

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

MACHI/APRILI 2013

Muda: Saa 2 $\frac{1}{2}$

Kidato cha 4

MTIHANI WA PAMOJA WA PENTAGON - 2013

WILAYA YA WARENG

Kiswahili

Karatasi ya 3

MAAGIZO

- Jibu maswali manne
- Swali la Kwanza ni la lazima
- Kisha chagua maswali mengine matatu kutoka sehemu zilizosalia.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- Kila swali lina alama 20

SEHEMU YA A. (LAZIMA) (alama 20)

Riwaya : Utengano - Said A. Mohamed

1. “Nimekosa ,nimetubu,sifanyi tena adabu niliyopata si ndogo.”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili . (alama 4)
- b) Eleza adabu iliyopata msemaji wa maneno haya. (alama 16)

SEHEMU YA B. TAMTHILIA (alama 20)

Mstahiki Meya – Timothy Arege

Jibu swali la 2 au la 3.

2. “Nirajua una shughuli nyingi ulizoziacha na kufuata wito wangu. Ni ukarimu mkubwa...”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Thibitisha kwa kutolea mifano mitatu jinsi msemewa amejawa na unafiki kwa kiwango kikubwa. (alama 6)
- c) Toa mifano mingine inayodhihirisha unafiki katika tamthilia hii mbali na ile ya msemewa. (alama 10)
3. Viongozi ni kielelezo cha ufisadi katika jamii. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea Tamthilia ya **Mstahiki Meya** (alama 20)

SEHEMU YA C. HADITHI FUPI (alama 20)

Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine – Ken Walibora na S. A. Mohamed (Wahariri)

Jibu swali la 4 au la 5

4. “Mja nisiye na shukrani.Nisiyefadhilika wala nisiyehisi... mbwa miye...”
- a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- b) Taja na utolee mfano tamathali mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili (alama 4)
- c) Eleza wasifu wa msemaji wa uneni huu. (alama 12)
5. Eleza vile mwandishi ameshughulikia swala la ubaguzi kwa kurejelea hadithi zifuatazo:
- a) Mke Wangu (Mohammed S. Abdalla)
- b) Damu Nyeusi (Ken Walibora)
- c) Maskini Babu Yangu (Ken walibora)
- d) Ndoa ya samani (Abu Marjan) (alama 20)

SEHEMU YA D. USHAIRI (alama 20)

6.

Mkata ni mkatika, harithi hatorithiwa,
Sina ninalolishika, wala ninalochukuwa,
Mlimwengu kanipoka, hata tone la murawa,
Mrithi nini wanangu?

Sina ng'ombe sina mbuzi, sina konde sina buwa,
Sina hata makaazi, mupasayo kuyajuwa,
Sina mazuri makazi, jinsi nilivyoachiwa,
Mrithi nini wanangu?

Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa .
Sina chembe ya majazi, mnoni kulaumiwa,
Nakwa'chemi upagazi, mgumu kwenu kutuwa,
Mrithi nini wanangu

Sina leo sina jana ,sina kesho kutwaliwa,
Hata nifanye la mana, mno ni kulaumiwa,
Poleni wanangu sana, sina kwenu cha kutowa,
Mrithi nini wanangu?

Sina utu sina haki, mila yangu meuliwa,
Nyuma yangu ila dhiki, na mbele imekaliwa,
N'nawana na mikiki, hadi n'tapofukiwa,
Mrithi nini wanangu?

Sina ila kesho kwenu , wenyewe kuiongowa,
Muwana kwa nyingi mbinu, mwende pasi kupumuwa,
Leo siyo kesho yenu, kama mutajikamuwa,
Mrithi nini wanangu?

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka .

(alama 1)

b) Taja na ueleze bahari zinazojitokeza katika shairi hili kwa kuzingatia:

i. Mizani

(alama 4)

- ii. Vina
- c) Andika ubeti wa nne katika lugha nathari. (alama 4)
- d) Taja na utolee mfano mmoja mmoja wa idhini ya ushairi iliyotumika katika ubeti wa tano. (alama 4)
- e) Taja nafsi – neni katika shairi hili. (alama 1)
- f) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
- g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi hili (alama 2)
- i. Shakawa
- ii. Upagazi

SEHEMU YA E. FASIHI SIMULIZI (alama 20)

- 7 (a) Eleza maana ya maigizo katika Fasihi Simulizi. (alama 2)
- (b) Eleza sifa **tano** za maigizo. (alama 10)
- (c) Eleza umuhimu wa maigizo katika Fasihi Simulizi. (alama 8)